



# UNASTAHILI HUDUMA ZA AFYA ZA BEI NAFUU

NY State of Health hutoa mipango ya afya ya bei nafuu na usaidizi wa kifedha ili kupunguza gharama zako. Pata usaidizi unaokufaa bila malipo, kutoka kwa wasaidizi ili uliganishe mipango na uchague mbinu ya kusimamia huduma inayokufaa zaidi.

## KATIKA NY STATE OF HEALTH 'UTAPATA

- 1 Mipango mingi ya afya bora unayoweza kumudu
- 2 Mipango iliyo na huduma za kuzuia magonjwa zisizolipishwa pamoja na kiasi cha chini cha malipo
- 3 Usaidizi wa moja kwa moja usiolipishwa wa kukusaidia kuchagua mpango wako
- 4 Usaidizi wa kifedha wa kukusaidia kulipia huduma zako
- 5 Essential Plan wa watu walio na mapato ya chini

## KUJISAJILI NI RAHISI! PATA MAELEZO HAYA KWA AJILI YAKO NA KILA MTU KATIKA FAMILIA YAKO

- ✓ Tarehe za kuzaliwa
- ✓ Namba za usalama wa jamii au, kwa wahamiaji wa kisheria, namba za nyaraka iwapo zipo
- ✓ Uajiri, rekodi za mapato, na Habari ya bima ya afya



**LINGANISHA MIPANGO NA UJIANDIKISHE LEO!**

1-855-355-5777 au

[nystateofhealth.ny.gov](https://nystateofhealth.ny.gov)

TTY: 1-800-662-1220

Msaada wa bila malipo wa kibinafsi

# THE ESSENTIAL PLAN

Essential Plan unafaa kwa watu wengi walio na mapato ya chini.

Kwa wengine, inagharimu chini ya dola moja kwa siku. Kwa wengine, haigharimu chochote.

**NA HAKUNA KIWANGO CHA KULIPWA AWALI,** kwa hivyo mpango huanza kulipia huduma zako za afya mara moja.

## ESSENTIAL PLAN HUTOA FAIDA ZIZO HIZO BORA KAMA TU MIPANGO MINGINE



Ziara za daktari, ukijumuisha wataalamu



Vipimo vilivyoagizwa na daktari wako



Maelekezo ya dawa



Huduma ya kulazwa na ya kutibiwa na kuondoka hospitalini

Chini ya Essential Plan, kiasi unacholipa kwa kila huduma ya afya – malipo ya kushirikiana na bima – kiko chini sana, wakati mwingine \$0.

Na huduma za kuzuia magonjwa hazilipishwi, ikiwemo ukaguzi na kuangaliwa mara kwa mara na daktari.



Jisajili kwa Essential Plan leo. Usajili upo wazi **MWAKA MZIMA.**